## 5. Ni njia zipi za kusuluhisha changamoto zilizotajwa?

(I) Kuupa kipaombele mradi.

(ii) Kuwe na mawasiliano ya uwazi.

(iii) Kushirikiana kwa wadau wote.

(iv) Uwazi kupitia ushirikiano

(v) Ratiba inayowafiki na kukubalika, sasisho za mara kwa mara (maelezo), mikutano ya mara kwa mara na wadau wote.

(vi) Kuwe na mwongozo maalumu na kulipa fidia kwa ardhi na ardhi au ardhi kwa fedha.

**HATUA 1**
MAHITAJI YA AWALI

**HATUA 2**
TAARIFA YA GAZETI SIKU 30

**HATUA 3**
TAARIFA YA GAZETI YA KUCHUKUA ARDHI SIKU 15 KABLA UCHUNGUZI

**HATUA 4**
- USAMBAZAJI WA TAARIFA
- UCHUNGUZI

**HATUA 5**
- KUPOKEA MADAI KUPITIA GAZETI ILIYOWEKWA NA TUME YA ARDHI
- KUSIKIZA KESI KUANGALIA UKUBWA
- NA ARDHI

**HATUA 6**
MAPENDEKEZO YA MALIPOKWA WALIOATHIRIKA

**HATUA 7**
- KUKUBALI MAPENDEKEZO YA MALIPO
- MALIPO KAMILI YA FIDIA MARAMOJA

**HATUA 8**
- FEDHA KULIPWA
- RIPOTI YA MARIDHIANO

**HATUA 9**
- UTAFITI WA MWISHO WA UKUBWA WA ARDHI
- MSAJILI WA ARDHI-PANGO KUFUNGIZA KATIKA SAJILI



Mhandisi Mwangi, Meneja wa mradi Kenya Water Security Climate Resilience Project, Dkt. Paul Daudi, mtaalamu wa vyuma Frontman Consultants na Bw. Sita Kangai wakiwa maeneo ya Chigato wakati wa uchunguzi wa NLC.



Mto wa Mwache iliyoko karibi na kijiji cha Chinguluni kuelekea baharini.



Kundi likijadiliana pamoja na PAPs



Uungaji wa kamati ya kurekebisha malalamisho katika eneo la Nunguni.



Irene Muchoki, Dkt. Mhandisi Kimaite, Mhandisi Mwangi, Mhandisi Kibachio, wote kutoka Kenya Water Security Climate Resilience Project walipotembelea maeneo katika Mazeras Field Off.



Makamishna wa NLC walipotembelea maeneo ya mradi, Kasemeni Kinango, jimbo dogo la kaunti ya Kwale.



Uchunguzi wa NLC katika maeneo ya Mnyenzeni.



Kamati ya PAPs Apex katika mkutano wa ufichuaji wa RAP katika eneo la Fulugani.

**Frontman Consultant Limited**
**S. L. P 171-80114 Mazeras**
**Nambari ya simu: +254 794 312299, +254 784 3333,**
**Jengo la Coast development Lobby Group**
**Mkabala na ofisi ya ACC Kasemeni**
**Mazeras – Kinango Road**
**Barua pepe: info@frontmancon.com,**
**Tovuti: www.frontman.com**

www.frontmancon.com

FRONTMAN Consultants — *The Group of Experts*

# KWSCRP MRADI WA BWAWA LA MWACHE

## Ni mchakato upi unaotumiwa kufidia ardhi?

Tume ya ardhi ya kitaifa (NLC) ina mamlaka ya pekee ya upatikanaji wa ardhi nchini kenya.serikali inapopata au kuchukua ardhi kwa minajili ya matumizi ya umma au maslahi ya umma,ardhi hiyo huthaminiwa na wenye ardhi hizo kufidiwa au kupewa sehemu nyengine za kuishi.Njia/Mchakato wa kawaida wa kuchukua ardhi (bila kuchelewa) huchukuwa miezi mitatu.
Kuna hatua tatu muhimu na kila hatua ina michakato yake.

## Kuhusu mradi wa Bwawa la Mwache

Serikali ya kenya kupitia kwa wizara ya maji,usafi wa mazingira na unyinyizaji maji, imepata ufadhili kutoka kwa benki ya Dunia chini ya mradi wa KWSCRP ambao unalenga kuzidisha usambazaji wa maji katika kaunti za Mombasa na kwale, pamoja na kuongeza maji na usafi wa mazingira katika kaunti yak wale .Mradi huu umenuiwa kuongeza mfumo wa kitaasisi wa kuimarisha usalama wa maji na hewa safi katika sehemu ya Pwani. Bwawa la Mwache ndio mradi ulioshika nanga katika uwekezaji na ulio mkubwa zaidi katika sekta ya maji.Tume ya ardhi ya Kitaifa ndiyo inayo shughulika upatikanaji wa ardhi kwa niaba ya serikali kuu na serikali za kaunti.Washauri wa Frontman wameajiriwa kusimamia uhamishaji wa watu walioathiriwa na mradi kupelekwa katika makazi mapya.

## 1. Hatua ni zipi?

### Hatua 1: Mambo ya kimsingi kabla ya uchunguzi

(i) **Ombi:** Tume ya ardhi ya kitaifa inapata ombi la kupata ardhi kutoka kwa shirika linalohitaji ardhi kupitia kwa mawaziri wa serikali au serikali ya kaunti.

(ii) **Mkutano wa ukaguzi:** Tume ya ardhi ya kitaifa huomba mkutano na wadau wanaotaka upatikanaji wa ardhi katika mkutano huo.Tume ya ardhi ya kitaifa hutaka orodha ya sehemu zilizoathirika na wenyeji wake.Pia hutaka maelezo ya hati za umiliki wa ardhi, ramani ya sehemu za ardhi zilizoathirika, njia mwafaka za uhamisho wa walioathirika kuwapa makazi mapya,ukifuatiwa na orodha ya watu wanaoathiriwa na mradi huo ili maombi yao yafikiriwe.

(iii) **Taarifa yenye nia ya kupata ardhi:** Taarifa inachapishwa kwenye gazeti rasmi la serikali baada ya tume kuthibitisha kwa maandishi kuwa ardhi inayotakikana kwa minajili au maslahi ya umma baada ya ukaguzi. Tume ya ardhi ya kitaifa inachapisha taarifa ya dhamira na kutoa nakala kwa msajili na pia kila mtu mwenye hamu ya ardhi hiyo.

### Hatua ya 2: Uchunguzi

(i) **Taarifa ya uchunguzi:** Tume ya ardhi ya kitaifa inaweka tarehe ya uchunguzi ambayo ni siku 30 baada ya kuchapisha taarifa ya kupata ardhi. Katika gazeti na siku 15 kabla siku ya uchunguzi, nakala ya taarifa itapewa kila mtu mwenye hamu ya ardhi hiyo.

(ii) **Kupokea madai:** Kufika siku ya uchunguzi malalamishi yote ya madai yakiwa katika maandishi hupokewa na Tume ya ardhi ya kitaifa .Kutokana na ukaguzi watu mahsusi walio na hamu ya ardhi hiyo hutambulika na madai yao kupokelewa.

(iii) **Usikilizaji wa kesi:** Kwa minajili ya uchunguzi,Tume ina uwezo wa kuwaita mashahidi wote pamoja na wote wenye hamu ya sehemu hiyo, Kuwaapisha, kuwa na makubaliano na kutoa uthibitishowa hati miliki za ardhi kwa Tume ya kitaifa. Hii inajumuisha wenyeji ambao ardhi yao imechukuliwa.

### Hatua 3: Baada ya uchunguzi

(i) **Kulipa fidia:** UBaada ya kutamatisha uchunguzi,Tume ya ardhi ya kitaifa hutengeneza vima tofauti ya malipoya fidia kwa kila mtu ambaye amethibitishwa na Tume kuwa mlengwa wa ardhi hiyo. Tume ya ardhi ya kitaifa baadaye humpa kila mtu anayelengwa taarifa ya malipo ya fidia.

(ii) **Ardhi iliyo katika sehemu ya kulipiwa fidia:** Tume ya ardhi ya kitaifa inaweza kukubaliana na mtu anayemiliki ardhi hiyo kuwa badala ya kulipiwa fidia, mtu huyo anaweza kupewa kipande kingine cha ardhi ambacho thamani yake haizidi fidia aliyostahili kupata. Baada ya kumaliza makubaliano hayo, mtu huyo huchukuliwa kuwa ameshalipwa fidia yake yote kuhusiana naardhi aliyokuwa akimiliki.

(iii) **Malipo ya fidia:** Baada ya kukubali mapendekezo ya malipo, Tume ya ardhi ya kitaifa huwalipa fidia walengwa wa ardhi hizo mara moja .Ikiwa mapendekezo ya malipo hayajakubaliwa au kunatokea utata wa ni nani anayefaakulipwa fidia, malipo hayo yanalipwa au kuwekwa kwa akaunti maalumu ya fidia inayowekwana tume ya ardhi kitaifa**.**

(iv) **Malipo ya riba:** Iwapo kiasi cha fidia hakikulipwa, Tume ya ardhi ya kitaifa wakatihuo au kabla kuchukua umiliki ,itafungua akaunti ili iweze kulipa riba kulingana na kiwango cha fidia iliyopendekezwa kulingana na viwango vya riba vya benki kutoka wakati wa kuchukuwa ardhi hiyo hadi wakati wa malipo**.**

(v) **Malipo ya ardhi ya ziada:** Ikiwa ardhi iliyochukuliwa ni kubwa kuliko kima cha ardhi kilicholipiwa, basi ardhi ya ziada italipiwa.

## 2. Ni stakabadhi zipi zinazohitajika kwa malipo?

**(i) Nakala ya tuzo/fidia.**
**(ii) Fomu ya ukubalifu iliyojazwa kikamilifu na kutia sahihi.**
**(iii) Fomu ya uhamishaji au utumiaji wa fedha kieletronikiau kwa benki iliyosainiwa na anayelipwa.**
**(iv) Nakala ya kitambulisho**
**(v) Nakala ya nambari ya Shirika la ukusanyaji ushuru nchini Kenya (KRA) na maelezo ya kina ya akaunti hiyo.**
**(vi) Uthibitisho wa umiliki wa ardhi.**
**(vii) Ruzuku iliyothibitishwa.**

## 3. Ni nini inafidiwa ardhi inapochukuliwa?

Kama ilivyo kulingana na sheria za kulipa fidia kulingana na kifungu cha sharia upatikanaji wa ardhi (CAP 295). Kifungu 295 sheria za Kenya, (ilivyorejelewa) kutathmini kinajumuisha:-

(I) Thamani ya ardhi na vilivyo ndani yake.
(ii) Hasara inayopatikana au inayoweza kupatikana au inayoweza kupatikana kutokanana kugawanywa kwa ardhi.
(iii) Hasara/uharibifu unaopatikana au unaoweza kupatikana kutokana na upatikanaji mbaya unaoathiri mali nyengine.
(iv) ***Gharama*** zinazopatikana kutokana na kubadilisha makaazi, biashara au ada za malipo ya kitaaluma.
(v) Gharama zinazopatikana kutokana na kupoteza biashara.
(vi) **Asilimia kumi na tano (15%) hulipwa kutokana na usumbufu.**

## 4. Changamoto zinazoweza kuchelewesha malipo kwa walioathirika?

(I) Mambo ya urathi au kesi
(ii) Hati miliki zilizotumiwa kama dhaman katika benki.
(iv) Mabishano na kutoelewana katika familia.
(iv) Ugawanyaji usio rasmi wa ardhi au hati miliki zilizokosekana
(v) Tamaa iliyokithiri ya walioathirkia.
(vi) Ugawanyaji ardhi ambao haujakamilika.
(vii) Rekodi zinazokosekana katika ofisi za usajili wa ardhi
(viii) Fidia ya ardhi inayo milikiwa na jamii